Arusha, Tanzania

Barua pepe: registrar@african-court.org
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-272-510-510

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**GODFREY GABINUS *AKIJULIKANA KAMA* NDIMBA NA WENGINE 2**

**DHIDI YA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 056/2019**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, 5 Juni 2026,** Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) leo imetoa hukumu katika kesi ya *Godfrey Gabinus Ndimba na Wengine 2 dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Waleta Maombi ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi) ambao, wakati wa kuwasilisha Maombi yao walikuwa wamefungwa katika Gereza la Wilaya ya Lindi Mkoani Lindi wakisubiri kutekelezwa kwa hukumu zao za kifo baada ya kushtakiwa na kukutwa na hatia ya mauaji. Waleta Maombi walidai haki zao zilikiukwa wakati kesi ikiendeshwa mbele ya mahakama za ndani.

Mahakama baada ya kubaini kwamba hakukuwa na maombi yoyote kwenye kumbukumbu kutoka kwa Mjibu Maombi, kwanza ilishughulikia suala la kutoa hukumu moja kwa moja. Kulingana na Kanuni ya 63(1) ya Kanuni za Mahakama (Kanuni za Mahakama), Mahakama ilibainisha kuwa masharti matatu lazima yatimizwe kabla ya kutoa hukumu moja kwa moja, ambayo ni: kwanza, Mhusika aliyepuuza apewe Maombi na nyaraka nyingine zinazohusiana na kesi; pili, Mhusika mmoja kupuuza kujibu; na tatu, ombi linalotolewa na Mhusika mwingine au Mahakama kuamua yenyewe.

Katika kutumia masharti haya, Mahakama ilibaini kwamba Mjibu Maombi alikuwa amepewa ipasavyo Maombi haya na nyaraka nyingine zote katika suala hilo na hivyo akaarifiwa ipasavyo kuhusu kesi hiyo. Kuhusu kupuuza kwa Mjibu Maombi, Mahakama ilibainisha kwamba Maombi yalikuwa yamewasilishwa kwa Mjibu Maombi ambaye hata hivyo alishindwa kuwasilisha Majibu ndani ya muda uliowekwa na kwamba hata baada ya kuarifiwa kwamba hukumu ya moja kwa moja itatolewa na

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-272-510-510



kupewa muda wa mwisho wa kuwasilisha Majibu yake, Mjibu Maombi hakuwasilisha maombi yoyote. Mahakama, katika mazingira hayo, ilihitimisha kwamba Mjibu Maombi alikuwa ameshindwa kutetea kesi hiyo ndani ya muda uliowekwa. Hatimaye, Mahakama ilibainisha kwamba ingawa Mleta Maombi hakuwa ameomba hukumu itolewe moja kwa moja, Kanuni ziliruhusu kutoa hukumu hiyo ama *kwa hiari* ya Mahakama au kwa kuombwa kufanya hivyo. Katika suala hili, Mahakama iliamua kutoa hukumu kwa msingi wa moja kwa moja *kwa hiari* ya Mahakama kwa ajili ya utoaji sahihi wa haki.

Ingawa hii ilikuwa hukumu ya moja kwa moja, hata hivyo, Mahakama, kwa mujibu wa Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za Mahakama, iliangalia vipengele vyote vya mamlaka yake ya kisheria ili kuhakikisha kwamba ina mamlaka ya kisheria. Kuhusu mamlaka yake ya kisheria, Mahakama ilihitimisha kwamba mamlaka yake yalithibitishwa ikizingatiwa kwamba Waleta Maombi walidai kuwa na ukiukaji wa haki zilizohakikishwa katika Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba) na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR), hati zilizoidhinishwa na Mjibu Maombi. Mahakama pia ilithibitisha mamlaka yake binafsi kutokana na kwamba Mjibu Maombi, kwa mujibu wa Kifungu cha 34(6) cha Itifaki, alikuwa ameweka Azimio kwenye Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki) ambayo Mjibu Maombi alitambua mamlaka ya Mahakama kushughulikia maombi yaliyowasilishwa dhidi yake na watu binafsi. Katika suala hili, Mahakama ilibainisha kwamba Mjibu Maombi kuondoa Azimio hilo mnamo tarehe 21 Novemba 2019 hakukuinyima mamlaka ya kisheria ikizingatiwa kwamba uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020 na haukuathiri maombi haya ambayo yaliwasilishwa mnamo tarehe 22 Oktoba 2019. Kuhusiana na mamlaka yake ya muda, Mahakama ilithibitisha mamlaka yake ikizingatiwa kuwa ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulianza baada ya Mjibu Maombi kuridhia Itifaki na kuendelea baada ya Mjibu Maombi kuweka Azimio. Mahakama pia ilithibitisha mamlaka yake ya kieneo ikizingatiwa kuwa ukiukaji wote unaodaiwa kufanywa ulitokea ndani ya eneo la Mleta Maombi. Kwa hivyo Mahakama ilitangaza kwamba ilikuwa na mamlaka katika suala hilo.

Mahakama iliona kwamba, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, lazima iamue kuhusu ukubalifu wa kesi zote zilizowasilishwa mbele yake. Ingawa ilikuwa hukumu ya moja kwa moja, Mahakama, ililazimika kuamua endapo Maombi haya yalizingatia matakwa ya ukubalifu yaliyowekwa chini ya Kifungu cha 56 cha Mkataba ambacho kimetajwa katika Kanuni ya 50(2) ya Kanuni za Mahakama.

Mahakama iliona kwamba kulingana na Kifungu cha 50(2) cha Kanuni za Mahakama, Maombi hayo yalitimiza masharti yafuatayo ya ukubalifu: Waleta Maombi walikuwa wametambuliwa kwa majina katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama; madai ya Waleta Maombi yalilenga kulinda haki zao kwa mujibu wa Kifungu cha 3(h) cha malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Maombi haya yalitimiza Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama; lugha iliyotumiwa katika Maombi haya haikuwa ya kutweza au kumtukana Mjibu Maombi au taasisi zake, katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama; na Maombi hayo pia hayakujikita tu kwenye habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari, katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusu kukamilisha taratibu za ndani, Mahakama ilibaini kuwa Waleta Maombi walikuwa wamekata rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa, ambacho ni chombo cha juu cha mahakama ya Mjibu Maombi, uamuzi wa Mahakama Kuu ukiwatia hatiani kwa mauaji. Mahakama ya Rufaa ilitoa uamuzi wake tarehe 28 Februari 2019, ikitupilia mbali rufaa ya Waleta Maombi. Kwa hivyo, Waleta Maombi walikuwa wamekamilisha taratibu za ndani kwa kuzingatia Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama. Mahakama iliona tena kwamba Maombi ambayo yaliwasilishwa miezi saba na siku 25 baada ya hukumu ya Mahakama ya Rufaa yaliwasilishwa ndani ya muda unaofaa kwa mujibu wa Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama. Mahakama pia ilijiridhisha kwamba Maombi haya hayakuibua madai ambayo tayari yalisuluhishwa mbele ya mahakama nyingine ya kimataifa. Matokeo yake, Mahakama ilitangaza kuwa Maombi hayo yanakubalika.

Kuhusu uzingatiaji wa sheria, Mahakama ililazimika kuamua endapo Mjibu Maombi alikuwa amekiuka Vifungu vya 1, 3, 4, 5, 7 vya Mkataba. Hata hivyo, kwa kuwa madai mengi ya Waleta Maombi yalihusu ukiukaji wa haki ya kusikilizwa kwa haki, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Mkataba, Mahakama ilishughulikia madai haya kwanza.

Kuhusiana na madai kwamba Mjibu Maombi alikuwa ameshindwa kuthibitisha uwepo wa Waleta Maombi katika eneo la uhalifu, Mahakama, huku ikitambua mipaka yake katika kutathmini maswala ya ushahidi yaliyowasilishwa mbele ya mahakama za ndani, iliona kwamba kumbukumbu ilionyesha kwamba Waleta Maombi walikuwa wametambuliwa kwa usahihi na walikuwa katika eneo la uhalifu. Kuhusu madai kwamba Mjibu Maombi alikuwa ameghushi ushahidi dhidi ya Waleta Maombi hasa kwa kupotosha ripoti ya uchunguzi wa maiti, Mahakama ilibaini kuwa haya yalikuwa madai ya jumla ambayo Waleta Maombi walikuwa hawajayathibitisha. Kwa hivyo Mahakama ilibaini kwamba Waleta Maombi walikuwa wameshindwa kuthibitisha

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-272-510-510



kwamba haki yao ya kusikilizwa kwa haki ilivunjwa kwa sababu ya madai ya kupotosha ripoti ya uchunguzi wa maiti. Kwa upande wa madai kwamba haki za Waleta Maombi zilikuwa zimekiukwa pale ambapo Mjibu Maombi hakumpa kila mmoja wakili wake na madai kwamba haki ya Waleta Maombi ya kuwadodosa mashahidi wa serikali iliathiriwa kwa sababu ya kutokuwepo kwa wakili binafsi, Mahakama iliona kwamba haki ya kutetewa na wakili si haki isiyo na masharti. Pia, Mahakama iliona kwamba jukumu la Serikali ni kumpa mtuhumiwa uwakilishi mzuri wa kisheria jambo ambalo si lazima lihitaji kwamba kila mtuhumiwa lazima awe na mwakilishi wake wa kisheria. Mahakama pia ilibaini kwamba hakukuwa na chochote kwenye kumbukumbu kinachoonyesha kwamba mwakilishi wa kisheria wa Waleta Maombi alikuwa ameathiriwa katika kuwawakilisha Waleta Maombi kwa pamoja. Mahakama ilibaini zaidi kwamba haki ya Waleta Maombi ya kusikilizwa kwa haki haikukiukwa kutokana na ukweli kwamba walikuwa na wakili mmoja anayewawakilisha wote. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi walikuwa wameshindwa kuthibitisha ukiukaji wa haki yao ya kusikilizwa kwa haki na hivyo ikatupilia mbali madai yao yote yaliyowasilishwa katika kipengele hiki.

Waleta Maombi pia walidai kwamba Mjibu Maombi alikuwa amekiuka haki yao ya kuwa na usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa wa sheria chini ya Kifungu cha 3 cha Mkataba. Walidai kwamba ukiukaji huo ulitokana na upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha wao kuwepo katika eneo la uhalifu; madai ya kuwasilisha ushahidi kinyume cha sheria katika mahakama za ndani; kushindwa kwa Mjibu Maombi kuwapa Waleta Maombi wakili binafsi; na wakili kushindwa kuwauliza mashahidi wa upande wa mashtaka baadhi ya maswali yanayohusu hatia ya kila mshtakiwa. Mahakama ilisisitiza kwamba ni wajibu wa mtu anayedai kufanyika ukiukaji wa haki ya usawa na ulinzi sawa mbele ya sheria kutoa ushahidi kuthibitisha madai hayo. Katika suala hili, Mahakama iliona kwamba Waleta Maombi walikuwa wameshindwa kutoa ushahidi wa kuthibitisha madai yao na hivyo kutupilia mbali madai yao.

Kuhusiana na madai ya Waleta Maombi kuhusu ukiukaji wa Kifungu cha 4 cha Mkataba, Mahakama ilibainisha kwamba Mahakama Kuu ya Mjibu Maombi ilikuwa imewahukumu Waleta Maombi adhabu ya kifo kutokana na sheria ya hukumu ya lazima. Kulingana na busara yake ya kisheria, Mahakama iligundua kwamba kutolewa kwa lazima kwa adhabu ya kifo kunakiuka Kifungu cha 4 cha Mkataba. Vivyo hivyo, Mahakama ilibaini kwamba utekelezaji wa hukumu ya kifo kwa kunyongwa unakiuka Kifungu cha 5 cha Mkataba.

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-272-510-510



Kwa kuzingatia ukiukaji wa Kifungu cha 4 na 5 cha Mkataba ambao ulikuwa umebainishwa, Mahakama pia ilibaini kwamba Mjibu Maombi alikuwa amekiuka Kifungu cha 1 cha Mkataba.

Kuhusu fidia ya kifedha, Mahakama haikutoa matokeo yoyote kuhusu hasara ya mali ikizingatiwa kwamba Waleta Maombi hawakuwa wameomba chochote katika suala hili. Kwa upande wa hasara ya kimaadili, Mahakama ilirudia kusema kwamba hasara hii inachukuliwa kuwa ilitokea katika kesi za ukiukaji wa haki za binadamu na iliamuru kwamba kila Mleta Maombi afidiwe Shilingi Laki Tatu (Sh. 300 000), kwa usawa.

Kwa fidia isiyo ya kifedha, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Waleta Maombi kuhusu kufuta kesi ya jinai na kubatilisha hukumu zao. Mahakama pia ilitupilia mbali ombi la Waleta Maombi kuhusu kuachiliwa huru ikisema kwamba hakuna mazingira ya kipekee yaliyokuwa yamebainishwa kuhusu kuhalalisha kuachiliwa kwao. Hata hivyo, ikizingatiwa kwamba Waleta Maombi walikuwa wamehukumiwa kifo kwa lazima, jambo ambalo Mahakama iliona kuwa ni kinyume cha Kifungu cha 4 cha Mkataba, hivyo Mahakama iliamuru Mjibu Maombi awafutie Waleta Maombi hukumu za kifo na awaondoe kwenye jela ya wanaosubiri kunyongwa. Pia Mahakama iliamuru kwamba Mjibu Maombi, bila kuchelewa, afanye marekebisho ya sheria zake ili kuondoa adhabu ya kifo ya lazima kwenye vitabu vyake vya sheria. Aidha, Mahakama iliamuru Mjibu Maombi achukue hatua zote muhimu, bila kuchelewa, kurekebisha sheria zake na kuondoa "kunyonga" kwenye sheria zake kama njia ya kutekeleza hukumu ya kifo

Mahakama pia ilimwamuru Mjibu Maombi achukue hatua zote muhimu, bila kuchelewa, kwa ajili ya kusikiliza tena kesi kuhusu hukumu ya Waleta Maombi, kupitia mchakato ambao unazuia kutolewa kwa adhabu ya kifo ya lazima, huku akiruhusu busara kamili ya afisa wa mahakama. Kwa kuzingatia hali ya sheria katika nchi ya Mjibu Maombi, hasa kuhusu adhabu ya kifo ya lazima, Mahakama iliamuru, ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea taarifa, kuchapishwa kwa hukumu hii kwenye tovuti za Mahakama, na Wizara ya Katiba na Sheria, na kuhakikisha kuwa hati ya hukumu inapatikana kwa angalau mwaka mmoja baada ya tarehe ya kuchapishwa.

Mahakama pia iliamuru Mjibu Maombi, ndani ya miezi sita baada ya taarifa kutolewa, awasilishe kwake ripoti kuhusu hali ya utekelezaji wa Hukumu hii inayoelezea hatua zilizochukuliwa na Mjibu Maombi katika kutekeleza Hukumu hii.

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-272-510-510



Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 28(7) cha Itifaki na Kanuni ya 70(3) ya Kanuni za Mahakama, Jaji Blaise Tchikaya na Jaji Dumisa B. Ntsebeza walitoa Maazimio kuhusu suala la adhabu ya kifo.

**Maelezo zaidi:**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na maelezo kamili ya Hukumu ya Mahakama ya Afrika,
yanapatikana kwenye tovuti: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0562019

Kwa maswali yoyote zaidi, tafadhali wasiliana na Msajili kupitia anwani ifuatayo ya barua pepe:
registrar@african-court.org

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na*
*Nchi za Afrika ili kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org*